




Zamani, wanyama waliishi pamoja.

Walikutana kumchagua mfalme.



Jimbi alitaka kuwa mfalme.

Alidanganya kuwa alikuwa na
moto kichwani.




Wanyama wengine
walimwamini Jimbi.

Walimchagua kuwa mfalme.



Msimu wa mvua ulifika.

Kila kitu kilikuwa maji na baridi.



Sungura aliuliza, "Tutaupata moto wapi tujipashe joto?"



Kima alisema, "Tutaupata kwenye kichwa cha Jimbi."



Wanyama walimtuma Mbwa
Mwitu kuleta moto kutoka kwa
mfalme wao.



Mbwa Mwitu alienda kuuchukua moto bila kumuamsha Jimbi.



Mbwa Mwitu aliweka nyasi kavu kichwani.

Hazikushika moto.



“Mwamshe mfalme Jimbi!
Tunahitaji moto sasa,” Mbwa
Mwitu alisema.



Jimbi hakuwa na moto wa kumpatia Mbwa Mwitu.



Kutoka siku hiyo, mbwa mwitu
hula jimbi.